

TANGU WAKATI HUO



Asante, Ndugu Herman. Nimekuwa tu nimeketi hapa nikikimeza, na, mwajua, ninakithamini sana.

² Na kabla hatujaenda mbele zaidi, nina hakika tulinii tu, hatukulitilia maanani. Nafikiri hiki kilikuwa ni maskini kiamshakinywa kizuri sana ambacho watu hawa walitupatia hapa, asubuhi ya leo. Nimekula viamshavinywa kote ulimwenguni, mwajua, katika mataifa mbalimbali, na hicho kilikuwa kiamshakinywa kidogo kizuri sana. Nami ninaamini ingekuwa, kwa kuwa sisi ni mabibi na mabwana Wakristo, kuacha kitu kidogo mezani kwa ajili ya maskini hao mabibi wazuri, jinsi walivyotuhudumia vizuri mwajua, kama mngekuwa na kidogo, mnajua. Ni desturi ya Marekani, nafikiri, kwamba tunawaachia kitu kidogo mezani.

³ Na jambo lingine, sipaswi kuwa nikisema hivyo, wakati hata sijalipia tiketi yangu mwenyewe, bado, lakini mimi... Ninawiwa na mtu fulani hiyo tiketi, kwa hiyo, na—nawazia. Kwa nini usikiweke tu kwenye sahani yako, na kuwaacha hao akina mama...? Hilo, hilo lingekuwa sawa? Loo, kiwekeni tu, baa... kabla hatujaondoka, kabla tu hatujaondoka, acheni tu kitu kidogo mezani.

⁴ Nami natumaini hawasikilizi, lakini, mnaona, tunatoa mfano, hebu na tuwe mfano. Mnaona? Na kwa hiyo, hebu na tuwe Wakristo halisi katika yote tufanyayo ama tusemayo, katika kila tendo, hebu na tuwe Wakristo halisi. Nami najua liko mioyoni mwetu, wakati mwingine tunaweza kusahau kwa urahisi mambo madogo kama hayo, lakini niliwazia tu ningetaja.

⁵ Ninaamini kuna Maandiko yasemayo, ni vizuri jinsi gani, au ni la thamani jinsi gani kwa ndugu kukaa pamoja kwa umoja, ni kama ma—mafuta yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyoshuka mpaka upindo wa vazi lake. Bila shaka tunaweza kusema hilo, asubuhi ya leo, kwa uaminifu halisi wa moyo, ya kwamba kwa kweli ulikuwa ni u—ushirika mzuri. Nimekuwa na mikutano mingi, nimeona mambo mengi kwa neema ya Mungu, sijawahi kukutana na kundi lolote la watu wazuri zaidi, ndugu halisi tu Wakristo, pamoja na sisi sote, tukiwa pamoja tu.

⁶ Ninajua hiki ni kiamshakinywa kidogo, lakini natumaini hili... Sasa, si mzaha, ni jambo lililotukia kweli, lakini ni kitu kidogo tu kinachoweza kubadilisha msimamo wa mawazo yetu kwa muda kidogo.

⁷ Ninapenda kuvua samaki. Nami hupanda juu sana milimani wakati mwingine kuvua samaki. Sasa, nina ndugu wengi sana hapa, ninajua, jambo lile lile, niliwaangalia tu wakiangaliana

basi. Kwa hiyo, dada, usibishane naye, mwache akavue samaki, hilo ni zuri kwake, yeye ni... nenda pamoja naye.

⁸ Nilimwambia maskini msichana wangu hivi majuzi, Rebekah, alisema, “Mimi... Nitakapolewa, kamwe sitaolewa na mwindaji.” Hmm! Kasema, “Ninaona yale ambayo mama yangu amepitia.”

⁹ “Hilo ni sawa, basi olewa na mcheza gofu, acha aende huko nje kwenye... huko nje pamoja na hao wanawake nusu uchi, na kadhalika, siku nzima, fanya hivyo.”

¹⁰ Akaliwazia, akarudi, kasema, “Unajua, Baba, imetokea tu kwamba nimebadilisha nia yangu.” Kasema, “Ninataka kuolewa na mhubiri, na nimwache awe mwindaji, halafu ninataka kuambatana naye.” Kwa hiyo, alikuwa ameyawazia yote. Vema.

¹¹ Nilikuwa nikivua samaki wakati mmoja, huko juu kabisa kaskazini mwa New Hampshire, hayo ndiyo makazi ya samaki aina ya traute, wa hudhurungi. Unawapata samaki wa kienyeji, walio juu sana, ni wapiganaji wazuri, lakini ha—hao wengine ni wa kufugwa, samaki wa kuanguliwa ni laini, na si wapiganaji sana. Kwa hiyo, nilikuwa nikiweka hema dogo mgongoni mwangu, na kutembea, labda, maili, matembezi ya siku tatu ama nne, huko juu kabisa kileleni mwa milima, ambapo wanapita mabwawa ya buku, na kadhalika, ambapo unafikia mahali alipo samaki halisi wa kienyeji.

¹² Na, loo, jinsi ninavyopenda kuwakamata jamaa hao wadogo! Nawakamata na kuwaachilia, ku—kuwakamata tu, hivyo tu, kujiburudisha tu. Huna budi kuwa na kitu cha kupumzikia, kwa hiyo, hasa sana katika huduma ya namna hii. Na, kwa hiyo Bw. Goad hapa, ananifundisha jinsi ya kutia risasi kwa mkono sasa, na kwa hiyo ninaendelea vizuri sana katika jambo hilo.

¹³ Kwa hiyo huko juu siku moja, nilikuwa na hema dogo la mtoto lililowekwa. Nami si mpishi mzuri, nisingeweza kuchemsha maji pasipo kuyaunguza, nawaambia, mimi—mimi ni mpishi mbaya tu. Lakini na—naweza kupika magole, ama, samahani, ni—ni—ninamaanisha *chapati maji*, mwajua, ndivyo tu—tunavyoziita. Vema sasa, tunaziita kila kitu, huko magharibi, tunaziita *vitambaa vya jasho*. Mnajua *kitambaa cha jasho* ni nini? Huingizwa chini ya matandiko ya farasi, mwajua.

¹⁴ Na kwa hiyo sikuzote tuliyaite, huko Kentucky, *magole*, na bila shaka, kwa kweli, ni *chapati maji*. Wala si lazima uchanganye chochote, zichanganye na maziwa haya ya unga kidogo, zichanganye, uzimwagilie. Na, bila shaka, nyote mnajua ya kwamba mimi ni, nilikuwa Mbaptisti, nami ninaamini katika kuzamisha, Sipendi kuzinyunyizia, kweli napenda kuzimwagilia, mwajua, kuzifunika tu vizuri sana kwa asali. Nami ninapenda asali, kwa sababu hiyo ni nzuri kwa maadili ya Kibaptisti, mwajua, wao, kama Yohana, mwajua, wanaokula

asali. Na kwa hiyo basi, nilikuwa na ndoo ya nusu galoni iliyojaa asali pale.

¹⁵ Basi asubuhi moja, huko chini kabisa kijitoni, nilikuwa na ma—mahali fulani, shimo pale, ambapo, pamejaa tu maskini samaki wa hudhurungi, wa kijito, yapata urefu wa inchi kumi na mbili, kumi na nne, na loo, walikuwa tu karibu kama kundi la nyumbu, mwishoni mwa mojawapo wa hizo nyugwe za kuvulia. Lakini kulikuwa na vichaka njiani mwangu, nisingeweza kurusha huyo nzi wa Mwanafarasi aende shoti vya kutosha, mwajua, kufika kule juu ambako . . . wangeweza kuona kivuli changu majini.

¹⁶ Kwa hiyo basi, nikachukua maskini kishoka changu na kushuka kule asubuhi hiyo, mapema, nikawazia, “Nitashuka na kufyeka hivyo vichaka, ili niweze kurusha ugwe na kurudi kule, na kuwatoa baadhi yao hao wakubwa kutoka chini humo, mahali hapo ambapo maji yalimwagikia.” Wao hurudi, wakajificha kwenye kilindi cha maji.

¹⁷ Kwa hiyo nikashuka, nikakikata, nikawakamata wachache, nami nilikuwa nikirudi, nikawaleta wawili kwa ajili ya kiamshakinywa changu. Basi kabla sijafika kwenye hema langu dogo, nikasikia kelele, na nchi hiyo imejaa maskini dubu hawa weusi. Loo, hawafikii . . . baadhi yao hufikia ukubwa mzuri sana, ratili mia tano ama mia sita. Lakini ilikuwa mwishoni mwa Mei, na kulikuwa—kulikuwa na maskini dubu jike, ama, ambaye, mama dubu, na watoto wake wawili walikuwa wameingia ndani ya hema langu.

¹⁸ Vema, si kile wanachokula, ni kile wanachoharibu, wanapenda tu kuharibu chochote. Kwa hiyo, nilikuwa na jiko dogo huko juu, la kupikia, walishuka tu chini, na kuchukua bomba hilo la jiko, na kurukaruka juu yake, namna *hiyo*, wapate tu kuisikia likipasuka, mwajua. Nao walikuwa wamerarua kila kitu kilichokuwa mle ndani. Halafu mmoja wao alikuwa ameipata ndoo yangu ya asali. Kwa hiyo, wanapenda chochote kitamu, mwajua.

¹⁹ Na kwa hiyo, nilipokuja, maskini huyo mama dubu alinisikia nikija, kwa hiyo, wao ni wepesi sana kusikia, ndipo akakimbia na kuwaita watoto wake. Vema, maskini jamaa hao wadogo warembo, na kwa kawaida wakati kitu kama hicho, huna kamera yako, unajua, kumpiga picha. Ndipo mtoto huyo mdogo, mmoja wa hao watoto wadogo akakimbia, huyo mwingine aliketi tu pale, vema, nikawaza, “Maskini jamaa huyo ana shida gani?”

Naye akaita tena, bali ha—hakuja, aliketi tu pale, ameinamisha kichwa chake. Nikawaza, “Loo, maskini jamaa huyo ana shida gani?”

²⁰ Vema, nilikuwa na shoka la kale mkononi mwangu, na maskini bunduki ya kale iliyoingia kutu imewekwa hemani, lakini nadhani ilikuwa imeraruliwa vipande-vipande wakati

huo, nami nisingetaka kumwua hata hivyo, kwa sababu ingewaacha mayatima wawili mweituni.

²¹ Kwa hiyo, nikawaza, “Vema, sasa . . .” Nami nikawazia mti, kwa sababu pamoja na hao watoto, yeye atakukwaruza, wajua. Kwa hiyo, ni—nikawazia, “Sasa, laiti ningaliweza tu kuona kile jamaa huyo mdogo anachungulia sana!” Alikuwa ninii tu . . . “Mbona?” Nikasema, “Mbona hakuja wakati mama yake alipomwita?” Kwa hiyo nikaendelea kupiga hatua *hivi*, huku nikitazama mti, kwa hiyo, nikitembea huku na huku, nikawaza, “Kuna nini?”

Nikasema, “Aisee, ondoka hapo!” Naye akakaa tu pale. Nami . . .

²² Maskini kitoto cha mama, na huyo mwingine huko, na huyo—na huyo mtoto na mama wanatembea wakiitana, mwajua, huku akimwita mtoto *huyu*, wala asingesogea. Nami nikawazia, “Sasa, kuna kitu fulani alichopata ambacho kinamvutia.”

²³ Nilipofika kando yake, maskini jamaa huyo alikuwa na ndoo yangu ya asali, naye alikuwa amelishika namna *hii*, na maskini unyayo wake, mwajua, naye amefungua kifuniko chake. Sasa, kweli hakujua jinsi ya kuila, kwa hiyo angechukua maskini unyayo wake, na kuingiza ndani namna *hii*, mwajua, na kulamba, na kulamba. Ndipo nikazunguka kando, nikamcheka, kidogo. Nami nikasema, “Ondoka hapo!”

²⁴ Ndipo akageuka na kuangalia, huku macho yake yamejaa *sana* asali, asingeweza kuniona, mwajua, naye alikuwa akipepesa macho pande zote, akiniangalia namna *hiyo*. Ilikuwa tu kote kwenye maskini tumbo lake, mwajua, amejaa asali kadiri alivyoweza kuwa. Nami nikawazia, “Kama hana yubile ya Kipentekoste, sijawahi kuona moja.” Hakuna hukumu, hakuna hofu, aliingiza tu mkono wake kwenye ndoo ya asali, akiramba tu.

²⁵ Vema, nafikiri hilo ni jambo ambalo tumekuwa nalo juma hili, hatujali ni nani anayesema lolote, hiyo ndiyo, sababu ya sisi kuwa Wapentekoste, hatujali hao wengine wanasema nini, tunamwabudu Mungu. Kwa hiyo, tumetumbukiza mikono yetu tu kwenye ndoo ya asali, kufikia kwenye viwiko vya mikono yetu, na tumekuwa tu tukiramba. Labda, hatuoni mbali sana, mwajua, bali tumejaa asali.

²⁶ Mnajua jambo la kushangaza juu yake, kuimalizia hadithi yetu ndogo, mnajua kilichotukia basi? Wakati, hatimaye, alipoilamba ndoo yake, nilikaa tu na kumwacha ajiburudishe, kwa hiyo, kwa hiyo baada ya kumaliza, aliyumbayumba akaondoka, akaenda kule, ndipo hao wengine wakamlamba. Kwa hiyo, kama hawakuhudhuria huo mkutano, watalamba, endelea tu kushuhudia. Naam, huyo mama na huyo mwingine walikuwa tu wakimlamba, upesi walivyoweza, walikuwa

wakipata, ninii tu, baadhi ya mabaki, mnaona. Kwa hiyo, lakini alikuwa ametumbukiza mkono wake kwenye ndoo ya asali.

²⁷ Ushirika, hakuna kitu kama huo. Mzee Dk. Bosworth aliniambia siku moja, akasema, “Ndugu Branham, unajua *fellowship* ni nini?” [Kiswahili: Ushirika—Mfa.]

Nikasema, “Nafikiri najua.”

Kasema, “Ni *jamaa* wawili katika *meli* moja.” Kwa hiyo, hiyo karibu ni sawa.

²⁸ Nina furaha sana kumwona jirani yangu hapa, asubuhi ya leo, yeye ni Ndugu Fred Sothmann, mmoja wa wadhamini wa kanisa langu, Ndugu Banks Wood, mdhamini mwingine wa kanisa letu, maskanini huko Jeffersonville. Laiti ninyi ndugu wawili mngesimama, kwa muda kidogo tu, tafadhali, Ndugu Fred, kama haitafanya . . . watu wapate kujua. Hao hapo wawili wa wadhamini wetu kanisani.

²⁹ Nasi tuna marafiki wengine hapa, wake zao na wapendwa wao wako hapa. Nami ningependa kutoa tamshi kuhusu Ndugu Wood, mke wake aliyeketi pale, ni majirani zangu. Bw. Wood ni mkandarasi, Bw. Sothmann ni mkulima kutoka Canada, Ndugu Welch Evans, aliyeketi *hapa* pembeni, ndugu mwingine mwaminifu. Hawa ndugu wawili wanaoketi *hapo*, mmoja Mkanada, huyo mwingine kutoka Georgia, wake zao hapa, wa—wao huendesha gari yapata maili elfu moja, kila upande, kila Jumapili ninapohubiri maskanini, huko ni kuja kwa uaminifu sana. Marafiki wazuri mno!

³⁰ Naye Bw. Wood akiwa ni mkandarasi, alikuwako, alilelewa katika familia aminifu ya Mashahidi wa Yehova. Naye alikuwa na mvulana kiwete, ugonjwa wa kupooza ulikuwa umeupinda mguu wake kabisa. Naye mkewe, nafikiri alikuwa mfuasi wa Church of God, Anderson Church of God, ama Methodist. Lilikuwa lipi, Dada Wood? Lilikuwa ni Anderson chur—...? Church of God.

³¹ Na kwa hiyo, walikuwa, mtu fulani alikuwa amewaambia nilikuwa na mkutano huko Louisville, nao wakashuka wakaenda kule, wakaona, usiku mmoja kule, mvulana mdogo aliyetolewa kwenye kiti cha magurudumu aliyekuwa na mtukutiko wa kupooza, naye akatembea hadi jukwaani, huyo jamaa mdogo alitiwa mafuta *sana* na Roho Mtakatifu, hata akahubiri jukwaani.

³² Msichana ambaye madaktari walikuwa wamemkatia tamaa, aliyekuwa na ugonjwa ule ambapo unageuka ukawa chaki. Naye alikuwa, juu sana kiunoni mwake, hakuwa amejongea kwa miaka minne au mitano, naye hapa akaamka kutoka kwenye hiyo machela, juu ya BWANA ASEMA HIVI, akakimbia huku na huku jukwaani, amesimama kutoka kila mahali, akiwa mzima kabisa, na mwenye afya.

³³ Mioyo yao ikaanza kumwonea Mungu njaa. Bw. Wood, wakati huo, akiwa mkandarasi, alikuwa na kazi iliyombidi kumalizia, upesi sana. Ndipo yeye na mke wake wakaenda Houston, Texas, ambako mhudumu wa Kibaptisti alitoa changamoto ya kufanya mjadala. Basi waache tu watoe changamoto, Mungu daima hulitekeleza vizuri kabisa. Huko ndiko ile picha ya Malaika wa Bwana ilipopigwa, hiyo, mnaona, Bw. Wood alikuwa yupo hapo Yeye aliposhuka.

³⁴ Nikatoka huko nikaenda Ufini, Uswidi, nchi za Skandinavia. Nilipokuwa njiani nikirudi, nilienda kwenye mji uliokuwa karibu na ambapo kijana *huyu* alimjia Bwana nilipokuwa nikihubiri. Huyu ni mmojawapo wa watoto wangu kutoka hu—hudumani, Ndugu Hill. Hiyo, nafikiri hiyo ilikuwa ni kweli, Ndugu Hill. Na kuwasikia hawa ndugu wengine, jinsi ambavyo mambo mbalimbali yalikuwa yametokea, nami ninazeeka sasa, na kwa hiyo, inanifanya niwazie juu ya hawa wavulana wadogo wanaokuja watapachukua mahali pangu baada ya kitambo kidogo, nina furaha sana kuwaona.

³⁵ Jambo moja ambalo nimetamani kuwa, ninapoona Assembly, Church of God, Pilgrims, na aina mbalimbali, Ni—ningekuwa tayari kusema asubuhi ya leo, kama vile Simeoni, “Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani,” wakati ningeweza kuwaona, moyo mmoja na nia moja, wakiungana tu pamoja.

³⁶ Shetani akiwafanya mshambuliane ninyi kwa ninyi, haimbidi kurusha risasi hata moja, mnaona, mnajipiga tu wenyewe, mnaona. Lakini nitakapoona lile Kanisa kuu la Mungu lililokombolewa likija pamoja, kama kundi moja kuu, nitakifunga Kitabu, kisha halafu nikirudishie mwanangu, Joseph, na kusema, pamoja na Billy, “Endelea, Mwanangu.” Watoto wangu wengine, wanangu, “Endeleeni mbele sasa, na mkae tu hivyo.” Ule Utawala wa Miaka Elfu utakuwa unaendelea wakati jambo hilo litakapotukia.

³⁷ Sasa, Bw. Wood alikuja kwa... Ndugu Wood, jina la mji huo huko Ohio lilikuwa lipi? Cleveland. Tulikuwa na mkutano mkubwa wa hema kule, na ilikuwa vigumu kwako kuukwepa. Na ninii yake, yeye akiwa ni Shahidi wa Yehova sasa, naye baba na mama yake ni Shahidi wa Yehova hodari, wote, baba yake ni msomaji. Naye akiketi huko nyuma kabisa mkutanoni alikuwa pamoja na maskini mvulana wake kiwete, Roho Mtakatifu akatokea. Nami sijui tu maneno aliyosema, ningesema kitu kama hiki kwamba, “Yule mtu kule nyuma aliye na mvulana ambaye... Na mke wake,” labda, “wanatoka Kentucky,” ama ninii, mwajua, jinsi anavyofanya kwa kawaida. “Ya kwamba huyo mvulana aliyekuwa na mguu uliolemaa sasa ameponywa, BWANA ASEMA HIVI.” Huyu mvulana hata hajui ulikuwa ni mguu gani, inambidi kuketi chini na kuichunguza, ulikuwa umenyoshwa *kikamilifu* sana. Mnaona?

³⁸ Naye ndugu yake akiwa ni Shahidi wa Yehova akashuka. Walimfukuza upesi sana alipofanya hivyo.

³⁹ Bw. Wood alisimamisha ukandarasi wake na kununua nyumba ndogo jirani yangu, naye ni, Mkristo wa Kipentekoste kweli. Sisemi kwamba hamna . . . kwa kuwa ameketi hapa, lakini wamekuwa majirani halisi, watu halisi. Nyumba yangu, kamwe sihitaji kuhofia chochote kuihusu, yeye yuko pale, endapo tu uwanja unahitaji kufyekwa, yeye huufyeka, na chochote tu namna hiyo, kusudi tu apate kuwa karibu.

⁴⁰ Ndugu Fred Sothmann, wengi wa hawa, Ndugu Tom Simpson, aliyeketi hapo, watu hao walitoka Canada, kusudi tu, wamepiga kambi huko nje, wamekuwa mle ndani kwa muda wa miaka miwili sasa katika trela, wapate tu kuwa karibu tunapokuwa na ibada. Loo, kile hilo, enyi marafiki, namna hiyo, kile linachomaanisha kwako! Sasa, ni adhimu kuwa na marafiki wa thamani.

⁴¹ Kwa hiyo ndugu ya Ndugu Wood, Lyle, akashuka akaja siku moja, nami nadhani, alitaka kumwuliza ni wa—wazimu wa aina gani aliokuwa amejihusisha nao. Na kwa hiyo, akasema, “Yule ndiye yule ndugu huko nje akikata nyasi katika mavuno.” Na huku nimevaa ovaroli yangu na kofia ya nyasi kavu. Nikaingia, nami nilikuwa nikizungumza naye.

⁴² Ndipo ikawa kwamba Roho Mtakatifu akakaribia, na kuanza kumwambia kuhusu yeye kuwa mtu aliyeoa, aliye na watoto wawili, na kadhalika. Kwa hiyo, a—akawazia, “Vema, Banks alimwambia hayo.” Nami nikashika hilo, kile alichowazia. Na kwa hiyo, watu wanaosema hivyo hawatambui ya kwamba unatambua kile wanachowazia. Mnaona? Wewe . . . Mungu hufunua tu kile kilicho moyoni mwao. Lakini, mnaona, wa—wao hawaninii, kweli hawaamini hilo.

⁴³ Kwa hiyo nikasema, “Lakini hili hapa jambo moja ambalo Banks hakuniambia, jana usiku, nusura upigwe risasi ya kichwa chako. Mke wako ambaye—ambaye umemwoa, bali ulikuwa na mwanamke mwenye nywele nyekundu jana usiku, naye akakuficha chumbani, na huyo ndiye aliyebishia mlangoni, nawe ukamtuma mlangoni, usingalifanya hivyo mtu huyo angaliulipua ubongo wako.” Hilo likamshika, alijua hiyo ilikuwa ni kweli.

⁴⁴ Tukaenda kuvua samaki pamoja chini bandarini, nasi tulikuwa tumeishiwa na chambo, na kwa hiyo tulikuwa tumeketi pale asubuhi moja, nilikuwa nikiwakamata maskini hawa mashavu bluu kama chambo kwa ugwe wa kuvulia usiku huo. Ndipo ndugu yake akasema . . . Nikasema, “Roho Mtakatifu yu karibu. Anataka . . . Kuna jambo fulani linalokaribia kutukia.” Nikasema, “Huenda ikawa, labda, ufufuo utatukia.” Nikasema, “Huenda ikawa, labda, nina yapata mia tano kwenye orodha kule, watoto wadogo, na kadhalika,” Nikasema, “labda, kitu fulani . . .”

⁴⁵ Ndipo ikatokea nikawazia, labda, kabla sijaondoka kulikuwa na... Samahani kwa hili, akina dada, sipendi paka, kamwe siwezi kuwavumilia. Na kwa hiyo, wao... Si—siwaogopi, lakini, loo, hisia hiyo ya msisimko wanayonipa! Kwa hiyo, wangeninii, msichana wangu mdogo akashuka kwenda njiani, naye pamoja na msichana mwingine jirani wakaja, naye akasema, “Loo, Baba,” mwajua, alikuwa na sura hiyo ya huzuni sana, akasema, “mtu fulani alimtupa nje ma—maskini paka, naye akala kitu fulani,” kisha kasema, “ni mahututi kabisa,” kasema, “a—amepewa sumu, atakufa.” Nami nikasema, “Baba, hungejali nikimchukua paka huyo, sivyo?”

Nami nikasema, “Vema, kama atakufa,” nikasema, “nadhani hatakufa.”

Kasema, “Waweza kumwombea?”

⁴⁶ Tulikuwa ndio kwanza tumemwombea maskini mbwa mdogo, mwajua, ambaye alikuwa tu yuafa, naye akapona, mbwa mkubwa, mzuri sasa. Kwa hiyo, nanyi mmesoma hadithi ya yule oposamu, na mambo hayo yote, hayo ni, loo, Mungu, huo ni uumbaji Wake, kama vile...

Kwa hiyo, nikasema, “Hebu nimwone huyo paka.”

⁴⁷ Kwa hiyo yeye na huyo msichana mwingine mdogo wakamleta nyumbani, nami nikasema, “Vema, naam, tutamweka, nendeni mkalete boksi.” Basi kesho yake asubuhi tulikuwa na yapata watoto kumi wa paka, mwajua, na kwa hiyo basi, kwa hiyo walikuwa nao.

⁴⁸ Kwa hiyo, mvulana wangu mdogo, Joseph, akatoka nje, naye akamtazama mmoja wao, naye ni jamaa mdogo tu, ndipo akambinya sana kupita kiasi, kisha akamtupa chini. Nami nikawazia alimwua huyo mnyama mdogo, akajipindapinda pale mara chache. Nikawazia, “Labda, ni mtoto huyo wa paka, mwajua, nitakaporudi, paka huyo atakuwa amekufa, kisha Bwana, amfufue tu.”

⁴⁹ Kwa hiyo, kesho yake asubuhi tulikuwa tukivua samaki, Bw. Wood pale, na mimi pamoja na ndugu yake. Tukaingia kwenye ghuba ndogo, nasi tulikuwa tukiwashika brimu wakubwa kiasi, mnavyowaita hapa, nafikiri, shavubluu, tunawaita huko chini Kentucky, milimani, huku upepo ukivuma, ilikuwa ni asubuhi nzuri.

⁵⁰ Naye Lyle alikuwa ameketi pale, si ugwe wa kuvulia, bali ndoana, alionekana kwangu kana kwamba alikuwa akitaka kuwashika nyangumi nayo, na alikuwa na mdudu ameuajaza *wadudu* kabisa. Akautupa kule, badala ya kuwakamata samaki, aliacha tu aiume, akaimeza ndoana moja kwa moja kwenye maskini tumbo lake. Ndi—ndipo alipomtoa, alisema, “Sasa, angalieni hapa niliyemkamata,” jamaa mdogo yapata urefu *huo*. Kwa hiyo akamkamata tu kwa mkono wake, tumbo limetolewa, mashavu, na kadhalika, jambo pekee aliloweza

kufanya, maana ndoana iliingia moja kwa moja kwenye maskini tumbo lake, badala ya kumkamata, mwajua. Nami nikasema . . . Ndipo akavuta nje maskini tumbo lake, na kumtupa nje majini namna *hiyo*, akasema, naye akatetemeka mara nne au tano, maskini mapezi yake yametandazwa, akasema, “Umepumua ya mwisho, ewe jamaa mdogo.” Naye kwa namna fulani ni mvulana mrefu wa mashambani, kitu kama hicho, hata hivyo.

⁵¹ Ndipo nikasema, “Sasa, Ndugu Lyle, unaona, kamwe usimruhusu samaki kumeza ndoana.” Nikasema, “Chukua tu chambo kidogo sana, na mara tu anapokigusa, umnase *hivyo*. Unaona?”

⁵² Nasi tulikuwa tumeketi pale tukizungumza, maskini jamaa huyo akalala pale juu ya maji kwa karibu nusu saa, ndipo upepo mwanana ukatokea na kumrudisha ukingoni. Tulikuwa tumeketi pale tukizungumza, na kuwakamata samaki hawa na kuwaachilia, sio kuwaua samaki, maana nilikuwa na angalau mia mbili au zaidi, nakisia, Ndugu Banks, kwenye ugwe, huko nje kwenye mishihi, kwa hiyo, tuliwakamata siku iliyotangulia, na kuwakatakata, tukawaweka kwenye ugwe.

⁵³ Lakini kuwaonyesha tu yale Mungu afanyayo, jinsi anavyojali kila kitu: Mara ghafula, kitu Fulani kikashuka kwenye vilima hivyo, kama upepo, nikasimama kwenye mashua. Yeye akasema, “Simama kwa miguu yako.” Nikasimama. Akasema, “Nena, na itakuwa hivyo.”

Nikasema, “Ati nini?”

“Huyo hapo yule samaki aliyekufa.”

⁵⁴ Nikasema, “Maskini ewe samaki mdogo, ninakupa uhai wako, katika Jina la Yesu Kristo.” Samaki mdogo akapinduka namna *hiyo*, akaenda akiogelea majini; amelala pale, na matumbo yake, yametolewa kinywani mwake, na mashavu yake.

⁵⁵ Sasa, Biblia hii imefunguliwa mbele yangu. Hiyo ni kweli, Ndugu Wood?

⁵⁶ Bw. Lyle Wood akaanguka tu kwenye mashua, akasema, “Hiyo ilimaanisha mimi, kwa sababu nilimwambia huyo samaki mdogo,” alikuwa amekufa yapata nusu saa, kasema, “Nilisema, ‘Umepumua ya mwisho.’”

Nikasema, “La.”

⁵⁷ Akasema, “Ndugu Branham, kwa nini Mungu atumie nguvu Zake kumfufua huyo samaki mdogo, na huku niliona kwenye kitabu hicho watoto kadhaa wenye kifafa? Sielewi hilo.”

⁵⁸ Nikasema, “Wakati mmoja Yeye alitoka nje ya mji wa Yerusalemu, ambamo kulikuwa na watu waliokuwa wamelala pale wakiwa na ukoma, na wakifa, na magonjwa yote, akaondoka, kisha akaona mti, haukuwa na chakula juu yake, ndipo akasema, ‘Ulaani huo mti,’ nao huo mti ukanyauka. Akatumia nguvu Zake kuulaani mti, huku watu wamelala huko

juu wakifa kwa mamia kwa ukoma, na magonjwa ya kila namna.”

⁵⁹ Inaonyesha tu ya kwamba Mungu anajali, haidhuru ni duni jinsi gani, ni wadogo jinsi gani, ni wakubwa jinsi gani, Yeye anawajali wote, maumbile Yake. Kwa hiyo kama makanisa yetu ni madogo, kama ni makubwa, kama wewe ni mlei, kama wewe ni mke wa nyumbani, kama wewe ni . . . chochote ulicho, Mungu anajua, Naye anakujali, na anajali yale unayomfanyia. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo tuna furaha asubuhi ya leo, kujua ya kwamba tunamtumikia Mungu kama huyo.

⁶⁰ Sasa, nina makaratasi yangu ya kodi ya mapato hapa chini kwenye ofisi ya posta, inafungwa nafikiri, saa tano asubuhi ya leo, kwa hiyo siwezi kuhubiri zaidi ya saa tatu, nina hakika. Kwa hiyo, mnisamehe kwa upumbavu wangu, nadhani. Lakini hata Mungu ana ucheshi, mwajua, kwa hiyo—kwa hiyo sisi . . .

⁶¹ Sina budi kusema jambo fulani ili kujiburudisha. Nanyi, hakuna mtu, ndugu yangu, dada, mpendwa, atakayejua yale maono hayo yafanyayo. Jana usiku, baada ya hiyo kuingia kwenye kusanyiko, kadiri ninavyokumbuka, yote yanaonekana kama ndoto kwangu, baada ya kutokea. Unapaswa kumfuata Billy Paul wakati mwingine, ama wale wanaopaswa kunipeleka, kunitikisa, na kunipiga teke chini ya goti, ama kuzungumza kuhusu kwenda kuvua samaki ama chochote kile, kuniondosha kwenye hilo. Sio wakati ukiwa *huko* juu, si wakati ukiwa *huko* chini, ni wakati ukiwa katikati. Unaona?

⁶² Halafu, kama vile nabii alipokuwa ametoa ujumbe wake, na—na kuagiza Moto kutoka Mbinguni, na—na mvua kutoka mbinguni, kisha akazunguka-zunguka nyikani kwa siku arobaini, ndipo Mungu akamkuta amerudi pangoni, mnaona. Ni hapo katikati, si wakati ninaposimama kama nilivyo sasa, si wakati ukiwa *huko* juu, unajisikia kana kwamba ungeweza kuupindua ulimwengu juu chini, bali ni wakati unapokuwa katikati ya nyakati hizo.

⁶³ Nami nafikiri watakuwa na dansi humu ndani, baada ya kitambo kidogo; natumaini tutafanya hivyo asubuhi ya leo, pia, dansi ya Kipentekoste, dansi ya Kipentekoste.

⁶⁴ Pia, angalieni, hilo ni jambo lingine ningetaka tu kusema miongoni mwa Wapentekoste, hili hapa jambo moja tunalosahau, enyi marafiki, ni heshima yetu ya Kipentekoste. Mnaona? Kuegesha katika sehemu za kuegeshea magari, wakati mwingine nimewaona ndugu zetu Wapentekoste, wakati kweli ungeweza kuingia, umpe mtu mwingine na—nafasi ya kuegeshea kando yako, wanaendesha tu kwa njia yoyote, inamfanya mtu . . . kwa kweli hufanya ninii, kile tunachoita *kuzomeana* barabarani, kushikwa na hamaki, na kushambuliana. Sikilizeni, hiyo siyo njia ya kuwa Mkristo wa Kipentekoste. Mnaona? Hebu na tumfikirie huyo mtu mwingine, kama amekosea, acha akosee;

kama ukimwiga, basi umekosea. Unaona? Hebu na tumfikirie jamaa huyo mwingine, mnaona.

⁶⁵ Na tujaribu tu kutenda mema, na kuwaza mema. Ninao msemu: “Tenda wema, huo ndio wajibu wako kwa Mungu, wazia mema, huo ndio wajibu wako kwako mwenyewe, nawe huna budi kutokea sawa.” Na kama utajaribu kufanya mema, unaona, yatastawi karibu nawe kama tu mzabibu, yatakukumbatia.

⁶⁶ Na kama huwezi kumpenda adui yako kadiri tu unavyowapenda wale wanaokupenda, kuna kasoro, mahali fulani. Unaona? Sasa, si kuwazia tu, “Ni wajibu wangu kumpenda adui yangu,” huna budi kumpenda kweli.

⁶⁷ Nilidhaminiwa na kundi la watu hivi majuzi tu, watu wazuri, sina neno dhidi yao, mawazo yao ni mawazo yao, siweki mipaka yoyote, lakini kundi hili la watu, makanisa sabini na mawili yalidhamini, nao wana njia—njia ya, wanabatiza kwa kuzamisha, kwa njia—njia ambayo hao wengine hawaamini katika kubatiza hivyo. Kwa hiyo mzee huyu mmoja wa wilaya akanipigia simu, na kusema, “Ndugu Branham, ulikuwa na mtu jukwaani, jana usiku, ambaye alibatizwa vibaya.”

Nami nikasema, “Vema, labda alibatizwa vibaya.”

Naye akasema, “Vema, tutachora tu mstari mdogo. Unapatana kupita kiasi.”

Nikasema, “Hebu kidogo,” nikasema, “ndugu huyo alikuwa na Roho Mtakatifu, sivyo?”

Akasema, “Vema, asingeweza kupata ondoleo la dhambi zake, kwa sababu hakubatzwa apate ondoleo la dhambi zake.”

Nikasema, “Lakini Mungu alimpa Roho Mtakatifu, kwa hiyo kama Mungu akimkubali namna hiyo, mimi pia namkubali.”

⁶⁸ Basi sikilizeni, afadhali nikosee Kimaandiko, na niwe na roho nzuri, kuliko kuwa sahihi Kimaandiko na kuwa na roho mbaya, mnaona, hiyo ni kweli. Ni kile kilicho *ndani* yako, kinajionyesha chenyewe. Unaona? Hicho ndicho... Uko nje... Maisha yako yanathibitisha kile ulicho.

Mtu huyu akasema, “Mimi... Tunachora duara ndogo, nasi tunakutoa kwenye duara zetu.”

⁶⁹ Nikasema, “Basi nitachora duara ndogo, na kuwarudisha ndani tena, unaona.” Kwa hiyo, mimi... Jambo ndilo hilo, kukurudisha moja kwa moja. Mimi... Hamwezi kunitoa nje, maana Mungu aliniweka ndani. Mnaona? Kwa hiyo ha—hamwezi kuniweka nje, kwa hiyo hivyo ndivyo tutakavyofanya. Mnaona? Aminini hilo.

Ninyi ni kundi zuri sana la ndugu.

Kibarikiwe kifungo kifungacho

Moyo yetu katika upendo wa Kikristo;

Ushirika wa watu wenye nia moja

Ni kama ule wa huko Juu.

⁷⁰ Hebu niwaambie hili, kama ndugu yenu . . . Na ndio kwanza nipite umri wa miaka ishirini na sita, hivi majuzi, mwajua. Mnajua hilo, siyyo? Nilimaanisha kwa mara ya pili. Mnaona? Kwa hiyo, sijui nitakuwa pamoja nanyi muda gani, sijui kuhusu hilo. Lakini hebu niwaambie siri ndogo, nguvu kuu kuliko zote ulimwenguni si kunena kwa lugha, wala kufasiri lugha, ama kupewa heshima na Mungu kuwa mhudumu, ama kuwa mwinjilisti, ama kuwa nabii, silaha yenye nguvu kuliko zote ambayo nimewahi kupata maishani mwangu, ni upendo. Utaninii. . . Upendo wa fileo, ambapo hilo neno la Kiyunani linatokana na *urafiki*, kama vile ulivyo nao kwa mkeo. Kuna tofauti. Itamfanya mama kwa ajili ya mtoto huyo mchanga, apitie kwenye ndimi za moto, maisha yake hayana maana, huo ni *fileo*. *Agapao* utafanya nini? Mnaona? Upendo wa kiungu.

⁷¹ Hatuna budi kupendana, kupendana Kiungu sisi kwa sisi, ndipo huoni kosa la ndugu yako. Kama akifanya kosa, wewe kamwe, angalia juu yake, nawe unampenda kwa vyovyote vile. Unaona? Jambo ndilo hilo. Ukiwapenda wale wanaokupenda, basi si mwenye dhambi hufanya jambo lile lile? Lakini wapende wale wasiokupenda, hilo ndilo linaloonyesha Roho wa Mungu yuko ndani yako, maana Yeye alikupenda ulipokuwa adui Yake, Naye akakupenda. Na ikiwa Roho huyo yuko ndani yako, atakufanya umpende adui yako, kama unavyompenda rafiki yako.

⁷² Tunaweza kuinamisha vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu? Baada ya mazungumzo haya yote madogo, kuninii, tungeweza kulishika Neno.

⁷³ Yehova mkuu, sisi ni watu wanaoelekea Umilele. Tunainamisha nyuso zetu kuelekea mavumbini tulimotolewa, na ukikawia, siku moja, mmoja mmoja, tutarudi kwenye mavumbi hayo, lakini kwenye Asubuhi hiyo ya ufufuo, tutakutana.

⁷⁴ Kama nilivyoangalia upande wa pili wa meza hii asubuhi ya leo, kama nilivyofanya katika mikutano mingi, niliangalia juu na chini ya mstari huu, na huko nje, nami nikaona watu, wahubiri wa Injili hapa, wameketi hapa, ambao labda, walihubiri Injili nilipokuwa mvulana mwenye dhambi. Kuna akina mama wakongwe wenye mvi hapa, ambao wamewapunguzia chakula watoto wao mezani kusaidea kujenga makanisa haya ambayo wavulana hawa wanawakilisha. Huenda nisiwaone tena baada ya mkutano huu kwisha. Huenda tusikutane tena kwenye kiamshakinywa katika dunia hii, lakini kuna jambo moja la hakika, tutakutana kwenye Chakula cha Jioni, wakati fulani, katika Nchi bora zaidi.

⁷⁵ Tunapowazia juu ya huo Mkutano mkuu angani, wakati meza hiyo kuu itakapotandazwa kwenye kanopi kutoka Umilele hata Umilele, na wote waliokombolewa wa nyakati

zote wameketi kuizunguka meza hiyo, nasi tunatazamana mezani, hapana shaka chozi dogo litatiririka mashavuni mwetu, tukiikumbuka mikutano hii na nyakati hizi, tupeane mikono mtu na mwenzake na kumshika kwa upendano wa ndugu na dada. Ndipo Mfalme mkuu atajitokeza, afute machozi yote kutoka machoni mwetu, na kusema, “Msilie, enyi watoto, yote yamekwisha. Ingieni katika furaha ya Bwana mliyowekewa tayari tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

⁷⁶ Baba, wakati kungali mchana, wakati tu—tukiwa duniani, na wakati tukiwa katika kipindi cha wakati, hebu na tufanye kazi kwa yote yaliyo ndani yetu, kumwingiza kila mtu mle tuwezaye akaketi katika ushirika huo mkuu.

⁷⁷ Wabariki watu hawa, ndugu hawa, hawa . . . baadhi ya hawa vijana, na wazee, na wanawake hawa, na watoto hawa wadogo, tunaomba ya kwamba utawabariki sana kwa nguvu na Uwepo Wako. Jalia mkutano huu ukue uwe uamsho mmoja wa kudumu, kutoka kanisa hadi kanisa. Jalia, mkono kwa mkono, na moyo kwa moyo, na tuweke juhudi zetu pamoja kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, mpaka tutakapomwona Yesu. Tunaomba hayo, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

⁷⁸ Katika Kitabu cha Mathayo, mlango wa 4, kifungu cha 17, tunasoma maneno haya:

Na tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni: kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.

⁷⁹ Nitachukua somo dogo, niangalie saa hiyo ya ukutani, somo la *Tangu Wakati Huo*.

⁸⁰ Sasa, zipo nyakati ambazo tunaweza kusema, “Tangu wakati *huo*.” Zipo nyakati ambapo kama mtoto mdogo, hawa wahudumu hapa wangeweza kusema, “Nilikuwa kanisani, na,” ama, “Nilikuwa huko nje kondeni,” ama, “Nilikuwa nikisoma Biblia, na tangu wakati *huo*.”

⁸¹ Mvulana mdogo, ama mzee, tuna wakati fulani ambapo jambo fulani linatukia, kisha tunasema, “Tangu wakati *huo*.”

⁸² Maskini mvulana huyo mdogo anaweza kusema, “Unajua, si—sikuwahi kusema uongo maishani mwangu, basi siku moja nikafanya msokoto wa gunzi la mahindi, ndipo nikaenda nyuma ya dohani ya moto, na—nami nikavuta sigara hii, kisha nikachukua kahawa, na kutia kinywani mwangu kusudi Mama asiinusi. Na—naye akasema, ‘Kadogoo, kwani umekuwa ukivuta sigara?’”

Taa nyekundu! “Usiseme uongo ewe kijana mdogo, usiseme uongo.” Dhamiri, “Usiseme uongo.”

“La, Mama.” Ulivunja kila kizuizi wakati huo. “Na tangu wakati huo, nikaanza kusema uongo.”

⁸³ Hivyo ndivyo tunavyoanza, hatuna budi kutia alama tangu wakati fulani, jambo fulani lilitukia, na tangu wakati huo, ilibadilisha mambo. Sote tuna nyakati kama hizo.

⁸⁴ Mwanamke mzinzi, akitembea mtaani, huenda alisema, “Wakati mmoja nilikuwa safi kama yungiyungi, na mwenye kumetameta kama baada ya mvua wakati umande wa mbinguni uliponiangukia, nami nilikuwa safi kama yungiyungi lile. Nilikuwa huko nje pamoja na mvulana ambaye nilidhani ni mwungwana. Usiku mmoja akanipa Coke iliyotiwa kileo, akanibusu kwa njia ambayo hakupaswa kunibusu. Badala ya kujiondoa kwake, na kumpiga kofi usoni, na kwenda nyumbani, nilijitupa mikononi mwake, na tangu wakati *huo*,” mnaona, daima kuna kitu fulani, “ndipo nikayatupilia mbali maisha yangu.”

⁸⁵ Nilizungumza na mwanamke kama huyo hivi majuzi, walikuwa wamempeleka kwenye wodi ya wagonjwa wa akili, nikaingia kumwombea. Wakasema, “Rudi.” Wamerukwa akili...Hivyo hasa ndivyo ingekuwa jana usiku. Maono yalikuwa yakiendelea moja kwa moja kuwaita hao watu kutoka kwenye vitanda vya wagonjwa na kadhalika, lakini wakati utukufu wa Mungu uliposhuka katika jengo hilo, nisingeweza hata kusikia tena.

⁸⁶ Mnajua ni kwa nini niliwatuma hao wahudumu kule chini? Nataka kusanyiko hili lijue, na watu hawa wajue nitakapoondoka hapa, kwamba si lazima waagizie ili nikawaombe, nilitaka watu wajue ya kwamba watumishi hawa wa Mungu wanaweza kuweka mikono yao juu ya wagonjwa. Si kitu cha mtu mmoja, ni kwamba sisi ni kundi la watu, sisi ni familia ya Mungu.

⁸⁷ Nikiingia kwenye chumba hiki cha dharura, kulikuwako na msichana mrembo ameketi pale, macho makubwa ya hudhurungi, na nywele nyeusi. Alionekana kana kwamba angekuwa malkia wa ikulu ya mwanamume yeyote. Kasema, “U hali gani?”

Akasema, “Njema, Ndugu Branham?”

⁸⁸ Nikaangalia kote, na hao hapo wamerukwa na akili, na kupiga mayowe, na kulaani, huku mwanamke mmoja akitumia maliwato ya kitandani, na kupangusa uso wake humo, na, samahani hilo, kwa ninii, baada ya kula kiamshakinywa chenu, lakini wendawazimu tu. Na hicho ndicho imani yako inacho... unapohubiri uponyaji wa Kiungu. Nikasema, “Vema, sijui kabisa nianzie wapi, kwanza.”

Ndipo huyo msichana akasema, “Laiti ungeanza nami kwanza, kama huninii...”

Nikasema, “Wewe si mgonjwa!”

Akasema, “Naam, bwana.”

Nikasema, “Vema, kwani kuna nini?”

⁸⁹ Akasema, “Bw. Branham, nililelewa katika nyumba ya Kikristo, nililelewa kumheshimu Mungu.” Akasema, “Wakati mmoja nilitembea na mvulana fulani, mama na baba yangu walinionya nisiambatane na mvulana kama huyo.” Lakini kasema, “Alikuwa anapendeza, alikuwa na, mwajua, nywele nzuri.”

⁹⁰ Na, loo, bila shaka, hilo ni—hilo ni sawa, hakika. Nami simlaumu mwanamke yeyote, onekana mrembo uwezavyo, na chochote kile, uwe safi, na mama, hilo ni sawa. Lakini ninachukia tu kumwona mtu akijibadili sura, wanawake hawa hata hawaonekani kama wanadamu. Mnaona? Mimi . . . Lakini kuonekana safi, kuwa kama mama wa heshima.

⁹¹ Nanyi wanaume, msiwe wachafu, huko si kunyenyekea, huo ni uchafu. Mnaona? Iweni safi, lakini msijaribu kuninii, mwajua, ni ninii tu, msijaribu kufanya mambo kama *hayo*. Kuwa tu ndugu wa kawaida, mnaona, na u—uwe tu wewe. Ninachukia kumwona mtu yeyote akijaribu kujifanya kitu ambacho kweli wasicho.

⁹² Samahani kwa kuacha somo hili kwa dakika moja. Nilikuwa huko Florida, ndipo mtu fulani akasema . . . Nilikuwa huko chini kumsaidia maskini mhubiri huyu, David, Little David miaka mingi iliyopita. Naye alikuwa ameingia katika mahali pagumu kule chini, nami nikashuka kwenda kumsaidia. Kwa hiyo, tulikuwa, Bwana alitupa umati mkubwa huko nje, na—na watu wengi sana, nisingeweza kuwatembelea wote. Kwa hiyo, mmoja wao akasema, “Duchess anataka kukuona.”

Nikasema, “Ati *nani*?” Sikuwahi kusikia jina kama hilo.

Kasema, “Duchess.”

Nikasema, “Vema, ni kitu gani hicho?”

Kasema, “Ni mwanamke anayemiliki mali hii yote kupitia hapa, alituruhusu kupiga hema hili hapa.”

Nikasema, “Vema, hebu waangalie tu hao mamia ya wagonjwa huko nje, wakijaribu kuniona, pia, kuwaombea.” Nikasema, “Kwani yeye ni mgonjwa?”

Kasema, “La, anataka tu kuzungumza nawe kwa muda kidogo.”

“Loo,” nikasema, “endapo nina wakati wowote, naomba niutumie pamoja na wale watu kule, ambao kweli wanauhitaaji.”

⁹³ Vema, wakamleta nyuma ya vipandio vya hema, ambapo nilishukia. Sasa, na—na—natumaini sisemi jambo lolote baya, mwanamke mkubwa mno amesimama pale akiwa na vito vya kutosha mikononi mwake ku—kumdhamini mmishenari mmoja mara kumi kote ulimwenguni, amesimama pale. Naye alikuwa na miwani, miwani, kwenye fimbo, na kuishikilia namna *hiyo*.

⁹⁴ Sasa, ninyi mnajua, nami najua, ya kwamba hutaangalia kupitia miwani yoyote namna *hiyo*, kuona chochote. Lakini ilikuwa ni kitu gani? Kujigamba. Mnaona? Naye akaangalia kupitia humo, akasema, "*Hivi wewe—wewe—wewe ni Dk. Branham?*"

Nikasema, "La, mama," nikasema, "Mimi ni Ndugu Branham."

Akanyosha mkono wake mbali sana *hivi*, naye akasema, "*Nimefurahi sana kukutana nawe.*"

Nikanyosha mkono, nikaushika mkono huo mkubwa, mnene, Nikasema, "Ushushe hapa chini, nipate kukutambua nitakapokuona tena," mnaona, namna *hiyo*. Kwa *hiyo* mimi—mimi. . .

⁹⁵ Mnaona, sasa, ilikuwa ni nini? Alikuwa tu akijaribu kuwa kitu ambacho hakuwa. Wewe ni nini hata hivyo? Futi sita za udongo, na ni hayo tu. Jina dogo tu la *Duchess*, ama—ama *Daktari*, ama—ama *Ph.D.*, ama *LL.D.*, hilo halina uhusiano wowote nawe, ni kwamba wewe ni kiumbe cha wakati duniani. Unaona?

⁹⁶ Sasa, msichana huyu, nilimwambia, "Tlikuwa?"

⁹⁷ Akasema, "Vema, mvulana mmoja, mvulana huyu alivuta sigara," kisha kasema, "alijaribu kunishawishi nivute sigara, wala nisingevuta." Kisha kasema, "Usiku mmoja alinipa kipande cha peremende, kilichokuwa *kimetiwa mkuyati*." Spanish Fly, ninyi madaktari wa mifugo, ama, madaktari mnajua hilo linamaanisha nini.

⁹⁸ Kwa *hiyo*, akasema, "Alinipeleka kwenye njia mbaya." Akasema, "Ndipo ni—nikatafuna peremende hii, nikifikiri ilikuwa sawa." Akasema, "Sijui kilichotukia mpaka kesho yake, na maadili yangu kama msichana yaliharibika." Kisha akasema, "Ndipo nikawazia, 'Kuna tofauti gani?' Nikaanza kunywa pombe."

⁹⁹ Akasema, "Nikajiunga na kanisa, nikafanya kila kitu nilichojua kufanya." Kisha akasema, "Basi hatimaye nilihudumiwa kwenye Makazi ya Mchungaji Mwema katika taasisi ya Katoliki, kisha nikajiunga na kanisa Katoliki, nikafikiri hilo lingenisaidia, halikunisaidia. Nilipotoka, nikafanya jambo lile lile." Kasema, "Nilikuwa kirukanjia, kahaba."

¹⁰⁰ Kasema, "Nilikunywa pombe, mlevi sugu." Kisha kasema, "Ndipo nilipoondoka huko," kasema, "wakanikamata tena, nami nikatumikia kifungo cha miaka miwili katika gereza la wanawake." Kisha kasema, "Nilipotoka kule, nikajiunga na kanisa lingine," kisha kasema, "halikufaa kitu." Naye akasema, "Ndipo nikasikia kuhusu mikutano yako, nilifikiri ningesuka nije huku, nione kama ungeweza kunisaidia."

¹⁰¹ Ndipo nikamwangalia, mwanamke mrembo, nami nikawazia, “Ati nini? Huyo si angekuwa ni malkia kwa maskini mwinjilisti fulani aliyechoka, akitoka hudumani, amechoka, maskini mke mwema, amkumbatie, aseme, ‘Mpenzi, najua umechoka.’”

¹⁰² Hamjui hilo linakufanyia nini! Sisi tunajua. Wakati nyakati zinapokwenda, hakuna mtu anayeweza kuchukua mguso wa mke mzuri sana. Sawa. Kama Mungu angaliweza kumpa mwanamume kitu bora zaidi, angalifanya hivyo.

¹⁰³ Nikawaza, “Jinsi angeweza kuwa maskini kitu kizuri!” Nikasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani. Hivi hukuwahi kamwe maishani mwako, kujisikia kana kwamba ungetaka kuwa na mume, na kupata watoto wachanga, na kuwa kama...?”

¹⁰⁴ Akasema, “Hakika, Bw. Branham,” akasema, “hiyo ingekuwa ndiyo shauku ya moyo wangu.” Vema, mwanamke hawezi kuwazia hilo na awe nje sana ya mstari, mwajua. Naye akasema, “Lakini ni nani angenichukua?” Akasema, “Mi—mi—mimi. . . Wewe ninii tu. . . Ha—hata nisingezungumza mbele ya mhudumu, mambo machafu, duni ambayo nimefanya,” na ninii, hata hivyo, msichana, labda ishirini.

Nami nikasema, “Vema, tunaweza kuomba?”

Naye akasema, “Ndiyo.”

Nikapiga magoti, nikasema, “Nataka uombe, nawe umwombe Mungu akusamehe mambo haya.”

Naye akasema, “Nimefanya hivyo mara nyingi sana, haifanyi kazi.”

Nikasema, “Vema, jaribu tena.”

Akapiga magoti akaomba, kisha akasimama, akasema, “Sasa, Ndugu Branham,” akasema, “Ninafungua ukurasa mpya, usiku wa leo.”

¹⁰⁵ Nikasema, “Naam, kisha uufunge tena, kesho,” mnaona, nikasema, “hilo halitafaa kitu.” Naye akasema. . . Nikasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani. Hutaki kufanya mambo hayo, siuyo, kipenzi?”

Naye akasema, “La, sitaki.”

¹⁰⁶ Nami nikasema, “Hili linaweza kuonekana la mtindo wa kale liwezavyo kuwa,” lakini nikasema, “huenda ukajiunga na kila kanisa, kila Methodisti, Baptisti, Katoliki, na kadhalika, utakuwa kitu kile kile.” Nikasema, “Ni pepo!”

¹⁰⁷ Hayo macho makubwa, maangavu yakaniangalia, naye akasema, “Bw. Branham, daima nimeamini hilo.” Kasema, “Kitu fulani kilinisukuma kufanya mambo ambayo sitaki kuyafanya.”

Nikasema, “Huyo ni pepo, nguvu za ibilisi.”

Naye akasema, “Daima nimeamini hilo.”

Kwa hiyo, nikasema, “Omba tena.”

¹⁰⁸ Akapiga magoti akaomba. Akaniangalia tena, nikamwombea, na kumwekea mikono. Na kwa hiyo, akakaa pale kwa muda kidogo, kisha akaangalia nyuma, akasema, “Unafikiri imekwisha?”

Nikasema, “Endelea tu kuomba.”

¹⁰⁹ Vema, akaomba kwa muda kidogo zaidi, nilikuwa nikichukua wakati mwingi sana pamoja naye, mpaka tu nilipomaliza kisa hicho. Baada ya kitambo kidogo akashika Moto, alipoushika, akasimama, na hayo macho yalikuwa yamebadilika, akasema, “Jambo fulani limetukia!”

Nikasema, “Sasa imekwisha. Haikubidi kujiunga na chochote sasa, Dada.” Ameolewa na ana watoto, hakuna kunywa pombe tena.

¹¹⁰ Rosella, uko hapa? Rosella Griffith, yule mlevi sugu, alikuwa kitu kama hicho. Ni wangapi wanaomjua Rosella? Wengi wenu, hakika, Rosella. Haya basi.

¹¹¹ Tangu wakati *huo*, jambo fulani, ndipo tangu wakati *huo* likabadilika. Hivyo ndivyo yule mwanamke mzinzi... Mlevi angeweza kusema, “Nililelewa kama mkataza pombe, watu wangu hawakuamini katika unywaji pombe. Lakini wakati mmoja nilikuwa pamoja na wavulana fulani, nao wakaniita dondoadume kama sikunywa pombe, ndipo nikanywa pombe yangu ya kwanza, na tangu wakati *huo*. Huo ndio wakati ulipoanza.”

¹¹² “Usiku mmoja katika—katika mkahawa wa barabarani, usiku mmoja tukiwa tumeegemesha kando ya barabara, wakati rafiki yangu wa kike aliponipa pombe, tangu wakati *huo* ikaanza.”

¹¹³ Mwaka Mpya, wao hufungua ukurasa mpya, nia njema, haifai kitu, hiyo haisaidii kitu. Nilizoea kumwona baba yangu akitupa tumbaku yake kwenye—kwenye Mwaka Mpya, na kusema, “Kamwe sitaitafuna tena,” kisha anaangalia mahali alipoitupa, kusudi aweze kuiokota kesho yake, mnaona. Nami nimemwona akitupa chupa yake, halafu naangalia kile alichofanya nayo, mnaona. Kwa sababu ninyi... Kufungua kurasa hakufai kitu, inahitaji jambo fulani litukie humo ndani.

¹¹⁴ Daktari yeyote atakwambia, kama ukiweka kitu kwa nje, na kuponya hicho kidonda, upande wa nje, itakifanya tu kibaya zaidi, kama hakijaninii... hakina budi kuponywa kutoka ndani, nje. Na hivyo ndivyo Ukristo ulivyo, sio kujiunga na kanisa, ama chochote kile, ni uponyaji kutoka *ndani*, kwenda nje. Uongofu wako unatoka ndani, kiini, roho, uhai.

¹¹⁵ Baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, wengi wenu ninyi vijana hamkumbuki jambo hili, sisi wazee tunakumbuka,

nilikuwa mvulana tu, umri wa miaka tisa, lakini ninakumbuka walisema, “Hatutakuwa na vita tena,” baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, “vyote vimekwisha. Walipata kitu kinachoitwa *gesi*, na sisi—sisi kamwe hatuwezi...ninyi... Kamwe hatutaweza ku—kunusurika vita vingine, kwa sababu ni...wao...Tutachukua wazo kwamba, ‘Kamwe hatutakuwa na vita tena.’ Hivyo tu. Tunavitatua milele.” Kwa hiyo, lakini walikuwa na vita vingine.

¹¹⁶ Ha—hatimaye waliunda kitu kilichoitwa, naamini kiliitwa *Shirikisho La Mataifa*, “Nasi tutachukua askari *kadhaa* kutoka katika kila taifa, pia tutakuwa na ulinzi wa polisi. Na kama mtu yeyote akikiuka sheria, mmoja wa hawa, *kadhaa* kutoka katika taifa hili, *kadhaa*...Tunaenda kusema, ‘Keti chini, John!’” Maana mataifa ni kundi tu la wavulana, familia tu, ni hayo tu, kama nyumba ya Mungu. “Nasi tutawachunga, na tutakuwa na *Shirikisho la Mataifa*.” Lakini walikuwa na vita vivyo hivyo.

¹¹⁷ Sasa, wana UN, bali tuna vita vivyo hivyo, mnaona, kwa hiyo...“Tutakapounda UN, na kuyaingiza mataifa yote ndani yake...Sasa, Urusi imetoka, na *hili*, na *lile*.” Mnaona? Hakuna moja ya mambo hayo. Hu—huwezi kuweka mikono yako juu ya hilo, hata kidogo.

¹¹⁸ Hao mume na mke vijana, wakati mmoja kulikuwako na mume na mke vijana, wangefunga ndoa. Nao hao mume na mke vijana huenda walisema, Yohana na Mariamu, na jinsi walivyoishi pamoja vizuri, nao huenda walisema ya kwamba “Mimi ni...”

¹¹⁹ Labda, huenda ikawa ninachukua muda mrefu kupita kiasi, na kuuchelewesha mkutano huu muda mrefu kupita kiasi. Inatupasa kuondoka saa ngapi, Ndugu? Huh? Saa ngapi? Loo, sikujua. Samahani, Ndugu. Dakika chache tu nasi...[Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam, bwana. Asante, bwana. Hatukujua hilo. Tulipaswa kuondoka saa nne.

¹²⁰ Hebu twende mbele kidogo tu. Yalikuwa mema na ya kupendeza, mpaka wakati mmoja maskini wauzaji, wenye nywele za mawimbi, walipoingia ambao walimshawhi kuingilia jambo baya, na kuivunja nyumba yake; tangu wakati huo.

¹²¹ Unasema, “Ndugu Branham, unatuambia asubuhi ya leo, ni mambo mangapi yanayotendeka, yale yanayotendeka, na yote *haya*, *yale*, na *mengineyo*, hivi kuna yoyote yanayoweza kutokea yanayosimama Milele?” Naam, wakati mtu anapokutana na Mungu.

¹²² Kulikuwa na mtu jina lake Ibrahimu, mtu wa kawaida tu, lakini siku moja alikutana na Mungu, na tangu wakati huo akabadilika milele. Aliamini *kitu* ambacho asingeweza kuona. Alipokutana na Mungu, alibadilika.

¹²³ Musa, mtumishi mtoro, hakuninii...alipaswa kuwakomboa wana wa Israeli, bali alitoroka, wala hakujua jinsi ya kufanya

hivyo, mafunzo yake ya kijeshi hayangemwezesha kufanya hivyo. Lakini siku moja, alikutana na Mungu, alikuwa ni mtu aliyebadilika. Basi mtu anapokutana na Mungu, inamfanya atende tofauti na alivyowahi kutenda. Ungeweza kuwazia nani, Musa...? Ni dhahaka jinsi gani, unapokutana na Mungu, yale itakayokufanya utende!

Billy, hivi ulisema tulikuwa na yapata dakika kumi? Dakika kumi, sawa.

¹²⁴ Ilifanyaje...? Hebu mwangalieni Musa. Hapa siku moja yeye ni mchungwa kondoo, mtawala wa Misri, mtoro, upande wa nyuma ya jangwa, huko nyuma upande wa nyuma ya jangwa, akichunga kondoo, akiogopa kwenda Israeli, ama kushuka kwenda Misri, hasa, naye huyu hapa upande wa nyuma ya jangwa, kesho yake asubuhi, huyu hapa pamoja na mkewe ameketi amemtagaa nyumbu, akiwa na mtoto nyongani mwake, masharubu yakining'inia chini *hivi*, mwenye umri wa miaka themanini, kichwa chake chenye upara kinang'aa, fimbo mkononi mwake, huyu hapa anaenda, "Utukufu kwa Mungu, haleluya," akitembea.

"Kwani unaenda wapi, Musa?"

¹²⁵ "Nashuka kwenda Misri kuiteka." Uvamizi wa mtu mmoja. Kwa nini? Alikuwa amekutana na Mungu. Mahali alipokuwa akipatoroka, sasa alikuwa anarudi kupateka, naye alipateka, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu. Na tangu wakati huo, kile kijiti kilichowaka moto, Musa alikuwa mtu tofauti, baada ya kukutana na Mungu, hiyo ni kweli.

¹²⁶ Mariamu, maskini yule bikira, kamwe mwanamke hakupata kuzaa mtoto, bila ya kuwa ni kujuana kimwili na mwanamume, hakuwahi kamwe, kamwe, hakuweza ku—kupata mtoto bila chavua ya asili, bali alimwamini Mungu, na kabla hajahisi uhai wowote, ama chochote kile, neno la Malaika lilikuwa zuri vya kutosha kwake, alikutana na Bwana. Kasema, "Salamu, Mariamu, umebarikiwa kati ya wanawake. Utapata Mtoto, pasipo kumjua mwanamume."

¹²⁷ Akasema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana." Na tangu wakati huo! Mariamu kamwe hakungojea mpaka alipokuwa na hakika. Kwa nini tungoje mpaka tuwe na hakika? Inatulazimu kuona mkono wetu ukinyooka, mguu wetu ukinyooka, maumivu ya tumbo yakikoma, si yeye, yule Malaika wa Bwana, ujumbe Wake ulikuwa mzuri vya kutosha kwake, akaanza kuzunguka, akishuhudia, "Haleluya! Nitampata Mtoto mchanga, pasipo kumjua mwanamume." Kwa nini? Alikutana na Mungu, hiyo ilikuwa ndiyo tofauti.

¹²⁸ Petro, alipokutana na Mungu, naye Yesu akamfunulia yeye alikuwa ni nani, tangu wakati huo alikuwa ni mtume.

¹²⁹ Paulo, maskini Myahudi mwenye pua iliyopinda, mwenye kejeli, akishuka kwenda kule pamoja na barua mfukoni mwake

kuwakamata watu wote wanaopaza sauti na kunena kwa lugha. Alikuwa anataka kuwafunga gerezani, alikuwa na agizo kutoka kwa kanisa kuu kufanya hivyo, bali alikutana na Mungu, na tangu wakati huo, loo, jamani, alikuwa ni mtu tofauti alipokutana na Mungu.

¹³⁰ Wakati mmoja mwenye ukoma mchafu, anayenuka alilala langoni, naye Yesu akapita, naye akasema, “Ukitaka, waweza kunitakasa.” Tangu wakati huo, hakuwa na ukoma. Kwa nini? Alikutana na Mungu, ndivyo ilivyo.

¹³¹ Mwanamke mzinzi alikutana na Mungu wakati mmoja kisimani, alikuwa na waume watano, huku akiishi na wa sita. Akamwambia siri yenyewe ya moyo wake, na tangu wakati huo alikuwa ni mjumbe wa Mungu kwa huo mji, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia yale nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹³² Unapokutana na Mungu, inabadilisha mambo, tangu wakati huo inabadilisha mambo, hakika inabadilisha. Inafanya hivyo kwa watu wote.

¹³³ Kulikuwa na kipofu wakati mmoja aliyekutana na Mungu, na tangu wakati huo angeweza kuona, bila shaka, mara alipokutana na Mungu.

¹³⁴ Sasa, tuna mengi zaidi tungeweza kusema, lakini kuharakisha, ninataka kutoa tamshi moja hapa: Mauti ilikutana na Mungu wakati mmoja, nayo kamwe haikuwa vile vile baadaye. Ibilisi daima alitilia shaka Huyu kuwa ni Mwana wa Mungu. Akawazia, “Kama huyo alikuwa Ndiye kule juu mlimani, kwa nini hakufanya mwujiza mbele zangu?”

¹³⁵ Wakati alipompeleka kule chini, na kumfunga kitambaa hicho machoni Mwake, na kumpiga kichwani, na kusema, “Kama wewe ni nabii, kama unaweza kuyatambua mawazo ya moyo, sasa hebu tuambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini,” waliwazia, “Hakika, huyo hawezi kuwa ni Mungu! Kumwacha mtu avute ndevu kutoka usoni mwake, na kukohoa na mate ya askari mlevi, na kumtemea mate usoni, na ati huyo awe ni Mungu, huku amesimama pale na asiseme Neno juu yake?” Kasema, “Huyo asingeweza kuwa ni Mungu. Mbona, Mungu angempiga afe!” Mnaona, yeye hajui kabisa tabia ya Mungu.

¹³⁶ Watu wengi hujaribu kuwa, “Mimi ni *Fulanii-wa-fulani*,” wanajitokeza namna hiyo, huyo si Mungu. Njia ya kushuka ni kupanda. Mnaona, mnaona? Wewe... Unyenyekevu Wake ulinithibitisha Yeye alikuwa ni Mungu, kile alichokuwa, mnyenyekevu, mtamu.

¹³⁷ Sasa, ibilisi alidhani Huyu hakuwa ni Mungu. Hebu tumwangelie tu wakati tu—tunapoangalia. Tuangalie jinsi mauti yalivyomkabili, na kile kilichoyapata mauti.

¹³⁸ “Huyo angeweze kuwa ni Mungu, akiwa ni mwanadamu? Mbona, alizaliwa huko chini nje ya ndoa takatifu. Mama yake labda alimzaa mtoto huyo kwa Yusufu, mzee huyu, mwenye umri wa miaka arobaini na mitano, naye kumi na sita. Mbona, yeye alikuwa ni baba wa watoto wanne ama watano, kisha aendeleo na kumwoa msichana huyu mdogo? Mbona, mtoto huyo mchanga alizaliwa nje ya ndoa takatifu.” Hivyo ndivyo ilivyowabidi kuigeuza, hivyo ndivyo hasa watu walivyoiamini. Alizaliwa chini ya . . . nje ya ndoa takatifu, waliamini hilo, mtoto haramu. “Huyo angeweze kuwa ni Mungu? Asingeweza kuwa ni Mungu.”

¹³⁹ Kwa hiyo ninamwona akipanda kilima, hebu—hebu twende Yerusalemu kwa dakika tatu zijazo, ama tano. Tunazungumza, nasikia kelele, hebu twende tukaangalie dirishani, tuliinue. Ninasikia kitu fulani kikienda, *bump, bump, bump*, ni msalaba wa kale, ukija mtaani. Alikuwa na vazi moja mgongoni Mwake, lililofumwa kote bila mshono.

¹⁴⁰ Umati unaopiga mayowe, ninamwona maskini mwanamke mmoja akikimbia mbele, akisema, “Kwani amefanya nini, ila kuwaponya wagonjwa wenu, kufanya waungwana kutoka kwa wahalifu wenu? Kwani amefanya nini, ila kutuletea matumaini ya Uzima?”

Mkono mkubwa, mgumu ukampiga mtaani, kasema, “Ungemsikiliza mwanamke huyo badala ya askofu wako, kuhani wako?”

“Kwani amefanya nini?”

¹⁴¹ Ninamwangalia, Yeye alikuwa mdogo, msalaba huo ukikokotwa. Ninaona madoa madogo mekundu nyuma ya koti Lake, ambalo ameliweka begani Mwake. Ni nini hayo? Huyo anapanda kilima. Hayo madoa yanaanza kuwa makubwa zaidi, na makubwa zaidi, makubwa zaidi, na baada ya kitambo kidogo, yote yanaingia katika sehemu moja kubwa, ni madoa makubwa sasa, ni Damu. Akikokota alama za miguu, anapopanda.

Ninaweza kumwona nyuki wa mauti akisema, “Unataka niende sasa, Shetani?”

¹⁴² “Naam, yeye—yeye, huyo si Mungu, hata si nabii, asingeweza kuvumilia jambo hilo, angelilaani kundi hilo la watu kama angekuwa ni nabii. Huyo si Yeye, endelea ewe nyuki, mchome, muume, tumempata sasa.”

¹⁴³ Ninaweza kumwona huyo nyuki wa mauti akianza kuvuma karibu Naye, akivuma karibu Naye. Ndugu, mtu yeyote anajua ya kwamba wadudu walio na mwiba kama vile nyuki, kama akiwahi kuchoma sana, hana mwiba tena. Aliuchomelea mwiba wake katika mwili mwingine basi, akauchomelea katika mwili wa Imanueli. Nyuki wa mauti alimchoma, mauti ikakutana na Mungu, tangu wakati huo, hana mwiba wowote. Aliuvuta mwili wake. Akamtoa nguvu. Asingeweza kuuma tena.

¹⁴⁴ Mtu mmoja jina lake Paulo, walipokuwa wakijenga ma—mahali fulani, jukwaa huko Rumi kukikata kichwa chake, nyuki huyo alianza kuvuma karibu naye, kutoa sauti, kasema, “Ee mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, Yeye atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

¹⁴⁵ Basi mauti ilipokutana na Mungu, Mungu alichomoa huo mwiba kutoka katika mauti. Jambo fulani liliipata mauti wakati ilipokutana na Mungu. Na, siku hizi, tunapoenda kukabiliana naye, mauti inaweza kulia, bali haiwezi kuuma, haina mwiba wowote.

Na tuombe.

¹⁴⁶ Baba, nina furaha sana kwamba kifo hakina mwiba. Kinaweza kufanya fujo, kuvuma kila mahali, na kujaribu kutuogopesha, lakini tunaweza kusimama kama Paulo wa kale, tumekuwa na ujuzi uo huo kwamba tumepita kutoka mautini, kwa sababu tumefichwa katika mwili unaoitwa Yesu Kristo, ambaye aliung’oa mwiba wenyewe wa mauti kutoka kwake. Kwa hiyo, tuna... Kaburi lenye matope haliwezi tena kumshikilia mwaminio, kwa kuwa Yeye alifufuka tena, na kama alivyofufuka, tunafufuka pamoja Naye, kwa kuwa wale waliokufa katika Kristo, Mungu atawaleta pamoja Naye katika Kuja Kwake.

¹⁴⁷ Mungu, kukiweko na mtu hapa asubuhi ya leo, ambaye hajawahi kukutana na Kristo, kama vile ningependa kulizungumzia, jalia wakutane Naye asubuhi ya leo, na maisha yao yatabadilishwa tangu sasa na kuendelea. Tujalie, Bwana.

¹⁴⁸ Sasa, tungeomba ya kwamba uwabariki wanawake hawa wazuri, waliotusaidia, na taasisi hii—hii ya chuo hiki cha Methodisti hapa, kwa heshima yao ya kuturuhusu kuchukua chumba hiki. Mungu, ninaomba ya kwamba vijana wanaume wanaotoka hapa watakuwa wamishenari halisi, na watu wa Mungu. Tujalie, Bwana. Jalia jambo fulani lifanywe ama kusemwa ambalo litaielekeza mioyo yao *sana* kwa Mungu, hata kutakuwa na akina John Wesley wa pili halisi kutoka hapa, Mungu. Tujalie.

¹⁴⁹ Wabariki washauri na kadhalika. Tubariki pamoja. Bariki ibada usiku wa leo, na ibada zijazo. Wabariki ndugu zetu wahudumu hapa, na wote waliokusanyika pamoja. Nasi tutakusifu, kupitia huu, wakati wetu, na Umilele. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁵⁰ Sasa, msisahau bakshishi za akina dada mezani, mkiweza. Basi Mungu awe pamoja nanyi, hata tutakapokutana, usiku wa leo. Vema. Mungu awabariki. 

61-0415B Tangu Wakati Huo
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org